





Khalai azungumza na mimea

- ✎ Ursula Nafula
- 👤 Jesse Pietersen
- 🗨️ Ursula Nafula
- 💬 Kiswahili
- 📊 Level 2






Khalai ni msichana mwenye umri wa miaka saba. Jina lake lina maana ya 'aliye mzuri' katika lugha yake ya Lubukusu.




Khalai anaamka na kuongea na mmea mchanga wa Mchungwa, "Tafadhali mti wa Mchungwa, kua mkubwa uzae machungwa mengi mabivu."




Khalai anaenda shuleni na njiani anaongea na Nyasi,
“Tafadhali Nyasi, kua kijani zaidi na zaidi na wala
usikauke.”



Khalai anayapita Maua ya mwituni na kusema,
“Tafadhali Maua, endelea kunawiri ili niweze kukuweka
kwenye nywele zangu.”



Akiwa shuleni, Khalai anazunguumza na Mti ulioko katikati ya shule, "Tafadhali Mti, toa matawi makubwa ili tusome chini ya kivuli chako."



Khalai anazunguumza na ua unaoizingira shule yake,
“Tafadhali ua, kuwa mwenye nguvu ili uzuie shule yetu
kutokana na watu wabaya.”



Anaporudi nyumbani alasiri, Khalai anautembelea mti wa Mchungwa kuangalia kama machungwa yameiva.



“Machungwa bado mabichi,” Khalai anashusha pumzi.
“Nitakuona kesho, we mti wa machungwa. Labda
utanipa chungwa bivu wakati huo.”



Storybooks Outline

global-asp.github.io/storybooks-outline

Khalai azungumza na mimea

Written by: Ursula Nafula

Illustrated by: Jesse Pietersen

Translated by: Ursula Nafula

This story originates from the African Storybook (africanstorybook.org) and is brought to you by [Storybooks Outline](#) in an effort to provide children's stories in the world's many languages.



This work is licensed under a Creative Commons
[Attribution 4.0 International License](https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/).